# Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia

**JESHI LA POLISI LA NSW LINAAHIDI KULINDA WATU WANAOTESWA NYUMBANI NA NDANI YA FAMILIA NA LITAWASHIKA WATU WANAOTENDA MAKOSA YA MATESO YA NYUMBANI NA NDANI YA FAMILIA.**

Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia ni jinai ya aibu inayoharibu usalama na furaha ya familia nyingi kupita kiasi katika NSW.

## Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia ni nini?

Kosa la mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia maana yake ni kosa binafsi hufanywa na mtu kushindana na mtu mwingine ambaye yule anayefanya kosa hilo ana uhusiano, au alikuwa na uhusiano wa nyumbani.

Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia yanamaanisha matendo yanayo husiana na: shambulio ya kimwili na kijinsia, matusi, kutengwa kwa kijamii, kunyimwa matumizi, kutesa kwa mhemuko, kuogofya na tisho, unyanyasaji na kuwinda. Kwa jumla wanaoteswa nyumbani na ndani ya familia kwa kawaida ni wanawake na wanaotenda kwa kawaida ni wanaume. Hata hivyo mateso ya nyumbani na ndani ya familia yanaweza pia kutendwa katika uhusiano wa jinsia na ushusiano wengine wa nyumbani.

Hayaizuia shambulio ya jinai tu. Ni pamoja na woga na hofu inayopita kwa watu wengi, hasa wanawake na watoto, kwa sababu ya matendo ya mtu fulani karibu kwao.

Hakuna mtu ambaye ana haki kufanya matendo hayo yoyote kwao. Hakuna sababu yoyote kwa Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia.

**Mtu yule ambaye anafanya kosa la Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia anaweza kuwa:**

- **mke au mume wa ndoa**
- **mwenzi au mwenzi umeachana naye**
- **bibi au bwana**
- **ndugu**
- **mtunzaji, mlezi au mtu ambaye anakaa katika nyumba moja**

## Nini inaweza kufanyikiwa?

Sheria la New South Wales inawapa polisi na mahakama uwezo wa kutoa ulinzi wa mara moja, kwa wakati wowote, siku au usiku. Ukijisikia unatishiwa au unahangaika juu ya usalama wa familia wako piga simu **Sufuri Tatu (000)**.

Polisi wanaweza kumshika na kumshtaki mtu yule anayekutesa au kukutisha wewe, au anayeharibu mali yako. Wanaweza kufanya ombi kwa niaba yako kwa Amri ya Kumkamata mtu akifanya Mateso ya Nyumbani (Apprehended Domestic Violence Order - ADVO) kukulinda kuzuia tisho na/au mateso mbeleni. Watoto na wateswa wa Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia wana haki ya kuishi kwa usalama katika nyumba zao.

ADVO ni amri inayofanywa na mahakama/korti kukulinda kuzuia madhara mbeleni. Amri hii inaweza kuwa pamoja na Amri ya Kuzuiliwa (Exclusion Order) inayokataa mtu wa mateso kurudi nyumbani. ADVO hii inawekea mipaka kwa matendo ya mtu unayeogopa – mtu huyo inaitwa mtuhumiwa.

Angalia mtandao wa polisi **www.police.nsw.gov.au** kwa habari zaidi kuhusu Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia.

# Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia

## Amri ya Kumkamata mtu akifanya Mateso ya Nyumbani

### Amri ya Kumkamata mtu akifanya Mateso ya Nyumbani (Apprehended Violence Order - AVO) ni nini?

**AVO ni amri kukulinda kuzuia mateso, tisho na unyanyasaji. Kuna aina mbili ya AVO, Apprehended Domestic Violence Orders (ADVO's) na Apprehended Personal Violence Orders (APVO's).**

ADVO ni amri inayofanyiwa na mahakama/korti kukulinda kuzuia mateso, tisho na unyanyasaji kutoka bwana au bibi, mwenzi, mpenzi, mpenzi aliyeachana, ndugu, mtunzaji, mlezi au mtu anayekaa nyumba moja nawe. APVO ni amri inayofanyiwa na mahakama kukulinda kuzuia mateso, tisho na unyanyasaji kutoka mtu yeyote usiye na ushusiano wa nyumbani au wa familia naye.

**Karatasi hii ya habari inaeleza ADVO tu.**

Kama una hofu kuhusu usalama wako unaweza kutoa taarifa kuhusu hofu yako na uzoefu wako wa mateso wa nyumbani kwa polisi na afisa wa polisi wanaweza kuomba ADVO kwa niaba yako. Maafisa wa Polisi **LAZIMA** waombe ADVO wakituhumu au wakiamini kuna kosa la mateso ya nyumbani, kumtesa mtoto au kosa la kuwinda/tisho limefanyikiwa au litafanyikwa kukupinga wewe.

ADVO inawekea mipaka matendo ya mtu unayeogopa (anaitwa mtuhumiwa) kwa njia ya kuweka masharti katika ADVO. Masharti hayo yanaweza kuwa:

- Asikushambulie, kukunyanyasa, kukutisha, kukuwinda au kukuogofya,
- Asiingie, kukaa au kufikia mahali popote unapokaa au kufanya kazi,
- Asikuwasiliane nawe moja kwa moja au kupitia mtu mwingine.

Masharti mengine yanaweza kutiwa ndani ikihitajika. Mahakama na Polisi la NSW inatunza kumbukumbu ya ADVO inayofanyikiwa Mahakamani na masharti yaliyoamuriwa.

Ni muhimu kutunza nakala ya ADVO yako nawe kila wakati. Kama mtuhumiwa haitii masharti ya ADVO, inaitwa uvunjaji. Piga simu kwa polisi kama mtuhumiwa anakiuka masharti yoyote ya ADVO. Polisi watachunguza uvunjaji na kumshtaki mtuhumiwa na uvunjaji ya ADVO kama kuna ushahidi wa kutosha.

Ni mahakama tu inayoweza kubadilisha ADVO's. Hakikisha masharti ya ADVO yanafaa kwa hali maalumu yako. Wewe au polisi mnaweza kuomba mahakama kubadilisha au kuondoa masharti au kurefusha ADVO kabla ya tarehe ya kumalizia, kama unaogopa mtuhumiwa bado.

### Ulinzi wa haraka

ADVO ya kitambo (au ya muda) yanaweza kuombewa kama unahitaji ulinzi wa haraka. Polisi wanaweza kuomba amri wa muda kwa ulinzi wako wa mara moja kupitia Jaji wa mamlaka masaa 24 kwa siku. Inawekea mipaka ya matendo ya mtu ili kukulinda kwa muda mfupi, mpaka jambo linaweza kusikilizwa mahakamani.

# Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia

## Je, ADVO inawapa watuhumiwa kumbukumbu la jinai?

Hapana. ADVO haimpi mtuhumiwa kumbukumbu ya jinai. ADVO inaandikiwa katika mfumo wa kompyuta ya polisi na tarehe ya kumalizika. Mtuhumiwa aliyekiuka ADVO na anaonekana na hatia ya kosa ile anaweza kupewa kumbukumbu ya jinai.

## Unahitajika kwenda mahakamani?

Ndio. Unahitajika kwenda mahakamani ili Mwamuzi anaweza kuamua kuhusu kufanya ADVO.

## Je, mtuhumiwa ataambiwa kwamba ADVO imeombewa?

Ndio. Kwa baadhi ya hali polisi wanaweza kuhitajika kuwasiliana na mtuhumiwa kuchunguza zaidi. Baada ya polisi wamefanya ombi, amri ya kuita mahakamani itatolewa kutoka mahakamani kumwamuru mtuhumiwa kwenda mahakamani kwa siku fulani kujibu malalamiko. Polisi watampa amri ya kumwita mahakamani pamoja na nakala ya malalamiko kwa mtuhumiwa.

## Je, ADVO itawalinda watoto?

Watoto wanaoathiriwa na Mateso ya Nyumbani & ndani ya Familia lazima walindwe. Watoto wako wanaweza kuwekewa katika ADVO yako au ombi la peke linaweza kufanyiwa kwa watoto wako.

Afisa wa polisi ni mtu pekee anayeweza kuomba Amri ya Kumkamata mtu akifanya Mateso kwa niaba ya mtoto chini ya umri wa miaka 16. Yeyote wa umri juu wa miaka 16 anaweza kuomba Amri ya Kumkamata mtu akifanya Mateso kwa niaba yake mwenyewe.

ADVO inaweza kueleza mtuhumiwa asikaribie watoto. Hata hivyo kama Amri ya Uzazi wa Sheria ya ipo inayoruhusu mtuhumiwa kuwasiliana na watoto, hii inaweza kupuuza masharti ya ADVO.

Kama kuna Amri ya Sheria la Familia (Family Law Order) inampa mtuhumiwa ruhusa ya kuweza kukaribia watoto na unaamini hawana usalama, inahitajika umwone mwanasheria au uwasililane na Makahama ya Sheria la Familia (Family Law Court) kupata ushauri.

## Siku yako makahamani

Tarehe unayohitaji kwenda mahakamani imeandikiwa kwenye ombi la ADVO. Labda utakuwa na maswali kuhusu taratibu ya mahakamani na mambo unayohitaji kufanya. Kwa usaidizi, uwasiliane na Afisa Ushirikiano na mateso ya Nyumbani (Domestic Violence Liaison Officer) kwa kituo cha polisi ya eneo lako, naye ataweza kukusaidia na kukuonyesha huduma nyingine.

Kwa habari unaweza pia kuwasiliana na Mahakama ya Eneo utakapoenda kuhuduria. Mahakama mengi pia yana huduma ya Usaidizi ya Mahakama ya Mateso ya Nyumbani inayoweza kukutolea habari.

# Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia

## Njia gani kutoa taarifa kuhusu Mateso ya Nyumbani na ya ndani ya Familia?

Kama wewe yupo hatarini ya sasa hivi piga simu Sufuri Tatu (000). Unapopiga simu Sufuri Tatu (000) mtumiaji simu atakuuliza unahitaji huduma gani. Sema tu 'Police', halafu unapojiunganisha endelea na umwelezea mfanyi kazi habari nyingi inavyowezekana. Ukipiga simu kutumia simu ya nyumbani au ya umma na unahitaji kuondoka kwa sababu ya usalama, acha simu ili mkono wake upo huru.

Kama hakuna hatari ya sasa hivi na ungependa kutafuta usaidizi au ushauri, uwasiliane na kituo cha polisi cha eneo yako. Kama hutaki kuongea na polisi mwanzoni, ndipo piga simu Laini ya Mateso ya Nyumbani ya DoCS (DoCS Domestic Violence Line), masaa 24 kila siku, siku 7 kwa wiki kwa nambari 1800 656 463.

Ni muhimu unapoongea na polisi uwajulishe mambo yaliyofanyikiwa na elezea hofu yoyote unayokuwa nawe. Waambie polisi ukifikiri mtu yule anamiliki au ana njia ya kufikia banduki au silaha nyingine.

Ukiwa mshahidi au una habari kuhusu tukio ya Mateso ya Nyumbani & ndani ya Familia, piga simu Sufuri Tatu (000) kwa jambo la haraka au kizushi. Kwa jambo la haraka wasiliana na polisi ya eneo yako au Crime Stoppers kwa namba 1800 333 000. Crime Stoppers ni huduma ya masaa 24 inayokuwezesha kutoa taarifa jinai bila kutambuliwa.

## Huduma za Usaidizi Support

Polisi la NSW lina Maafisa wanaohusikiana na Mateso ya Nyumbani zaidi ya 100 (Domestic Violence Liaison Officers - DVLO), ambao ni wataalamu wa kushughulikia na maswala ya Mateso ya Nyumbani na ndani ya Familia.

Maafisa ushirikiano Mateso ya Nyumbani wanaweza:

- Kuhakikisha unapata habari sahihi kuhusu taratibu ya sheria juu ya ADVOs
- Elezea haki yako na jibu maswali yako
- Kwenda mahakamani nawe
- Panga nawe ili unaweza kuwasiliana na huduma maalum ya eneo unapozihitaji.

### Mashirika Masaa 24, siku 7 ya wiki

**DoCS Domestic Violence Line**
**Laini ya DoCS Mateso ya Nyumbani**
- Piga simu 1800 656 463 (bure)
- TTY 1800 671 442*
- www.community.nsw.gov.au

**Victims Support Line**
**Laini ya Usaidizi wa Wateswa**
- Sydney mjini (02) 9374 3000
- Piga simu NSW 1800 633 063 (bure)
- TTY 9374 3175*
- www.lawlink.nsw.gov.au

**NSW Rape Crisis Centre**
**Kituo cha kipeo cha kubakwa NSW**
- Piga simu 1800 424 017
- www.nswrapecrisis.com.au

**Women's Health Centres**
**Vituo vya Afya ya Wanawake**
- www.whnsw.asn.au

**DoCS Helpline**
**Laini ya Usaidizi DoCS**
- Piga simu 132 111
- TTY 1800 212 936*

**Law Access NSW** (9am – 5pm, saa 3 asubuhi mpaka saa 11 jioni, Jtatu mpaka Ijumaa)
- Piga simu 1300 888 529
- www.lawaccess.nsw.gov.au

*TTY (kwa wapiga simu wanayokuwa na ulemavu wa kusikia).

CRIME STOPPERS
1 800 333 000
www.crimestoppers.com.au

Polisi, Moto, Ambulensi
**Sufuri Tatu (000)**
Katika dharura

Crime Stoppers
**1800 333 000**
Toa taarifa ya jinai bila kutambuliwa

NSW Police Force
www.police.nsw.gov.au